

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## HALMASHAURI YA WILAYA LUSHOTO



22/09/2021

ZABUNI NA; LGA.130/2021/2022/HQ/01


## TANGAZO LA KUTOA HUDUMA YA CHAKULA.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto anawatangazia Wananchi wote fursa ya kutoa huduma ya chakula katika Jengo la Halmashauri ya Wilaya Lushoto.

### **MASHARTI YA MWOMBAJI.**

- i. Mwombaji anatakiwa kuandika barua akitaja Bei/Kiasi atakachoilipa Halmashauri kwa kila mwezi kwa utoaji wa huduma ya chakula katika jengo kuu la Halmashauri ya wilaya Lushoto.
- ii. Mwombaji (kama atahitaji kuona eneo la kutolea huduma) amuone Afisa Biasharawa Halmashauri kwa ajili ya kujionea mazingira na eneo la Canteen itakayokodishwa.
- iii. Mwombaji anatakiwa kuwa na leseni ya biashara pamoja na TIN namba.
- iv. Mwombaji atatakiwa kuwa na Samani (viti na meza) za kutosha zitakazomuwezesha kutoa huduma hiyo kwa ufanisi.
- v. Mwombaji atatakiwa kuwa na vyombo vya kutosha (sahani, vikombe, vijiko, warmer n.k.) vitakavyomuwezesha kuwahudumia wateja kwa urahisi na kwa ufanisi mkubwa.
- vi. Mwombaji hataruhusiwa kutumia kuni wakati wamaandalizi ya chakula cha wateja.
- vii. Mwombaji atatakiwa kuzingatia usafi wa hali ya juu wa Canteen wakati wote wa kutoa huduma ya chakula.

- viii. Mwombaji atatakiwa kufika ofisi ya Ugavi na Manunuzi kabla ya kulipa ada ya maombi ili kupata fomu ya orodha ya vyakula vinavyotakiwa ili mwombaji ajaze bei kabla ya kutuma maombi.
- ix. Mwombaji atatakiwa kulipa Ada ya Maombi Tshs. 50,000/= (Elfu Hamsini tu.), baada ya kupata fomu ya orodha ya vyakula kutoka ofisi ya manunuzi. Hivyo Mwombaji anatakiwa kufika ofisi ya Mweka Hazina wa Halmashauri ya Wilaya Lushoto na kiasi tajwa hapo juu kwa ajili ya kufanya malipo ya zabuni hiyo. Fedha hizo hazitarudishwa.
- x. Maombi hayo yanatakiwa yatumwe kwenye bahasha iliyofungwa kwa ***lakiri***yakiwa na barua ya maombi pamoja na fomu orodha ya vyakula iliyojazwa bei.
- xi. Bahasha ya Maombi itumwe kwa: **Katibu wa Bodi ya Zabuni Halmashauri ya Wilaya Lushoto, S. L. P. 32 LUSHOTO.**
- xii. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **04/10/2021** saa **9:00** JIONI na zabuni zitafunguliwa katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kuanzia saa **9:30** JIONI siku hiyo hiyo. Waombaji/wawakilishi wote wa Zabuni watakaopenda kushuhudia ufunguzi huo wanaombwa kuhudhuria.



-----  
**EMMANUEL D. VURI**  
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**LUSHOTO**

**KURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**LUSHOTO**